# TANGAZO

## MAHAFALI YA 19 KATIKA CHUO CHA BAHARI DAR ES SALAAM.

Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) anapenda kuwatangazia wahitimu na wadau wote kuwa, Mahafali ya 19 ya Chuo cha Bahari, yanatarajiwa kufanyika tarehe 30 Novemba, 2023 kuanzia saa nne asubuhi katika viwanja vya chuo cha Bahari. Mahafali yatatanguliwa na kongamano la kitaaluma (Convocation) litakalofanyika tarehe 29 Novemba, 2023 kuanzia saa tatu asubuhi. Wahitimu waliowahi kupata elimu na mafunzo katika Chuo cha Bahari (DMI Alumni) na wadau wote wanakaribishwa kushiriki kongamano hili.

Wahitimu wote mnakumbushwa kuzingatia muda wa kuanza mahafali. Aidha, mnakumbushwa kuanza kulipia majoho kuanzia tarehe 21/11/2023 kupitia namba za malipo zifuatazo;

Wahitimu wa Astashahada na Stashahada **NAMBA YA KUMBUKUMBU YA MALIPO – 994410098339**

Wahitimu wa Shahada na Shahada ya Uzamili. **NAMBA YA KUMBUKUMBU YA MALIPO – 994410098338.**

Majoho yote yanapatikana Chuoni, Ofisi ya manunuzi kwa gharama ya Ths. 20,000 wahitimu wa Astashahada na Stashahada, na Tshs. 40,000 kwa wahitimu wa Shahada na Shahada ya Uzamili.

Kauli mbiu ya mahafali ya 19 ni "Kufungua fursa za Uchumi wa Buluu Jumuishi: kuwezesha Elimu ya Bahari na Mafunzo".

**WOTE MNAKARIBISHWA**

19 Barabara ya Sokoine, S.L.P 6727,Dar es Salaam, Simu/Nukushi:+255 222 126 988,
Barua pepe:info@dmi.ac.tz,principal@dmi.ac.tz,Tovuti:www.dmi.ac.tz
*"Chuo Bora katika Elimu na Mafunzo ya Bahari"*